JARIDA LA RS RUVUMA

TOLEO LA AGOSTI , 2026

RUVUMA YETU

Na. 0004

Tembelea ;www.ruvuma.go.tz

RUVUMA IVUME KWA MAENDELEO



BWAWA LA NYERERE CHACHU YA UWEKEZAJI RUVUMA

Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere lenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115 linatajwa kuongeza upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini, hatua inayotarajiwa kufungua fursa mpya za uwekezaji na maendeleo ya viwanda katika mkoa wa Ruvuma na taifa kwa ujumla.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amesema Ruvuma ni miongoni mwa mikoa inayochangia maji yanayoingia kwenye bwawa hilo, akitoa wito kwa wananchi kutunza mazingira kwa kutochoma misitu, kulinda vyanzo vya maji na kutumia rasilimali kwa njia endelevu.

Amebainisha kuwa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo uchimbaji wa Uranium wilayani Namtumbo inahitaji umeme wa uhakika, na sasa mazingira ya uwekezaji yameimarika. Vilevile, huduma za kijamii kama hospitali, shule na vituo vya afya zitapata umeme wa kudumu, hatua itakayoboresha maisha ya wananchi.

RC Ahmed amesema kutokana na malighafi nyingi za kilimo kama kahawa, mahindi, soya na mazao ya misitu, uwepo wa umeme wa uhakika unatarajiwa kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani ya mazao hayo na kuongeza ajira kwa vijana wa Ruvuma.

Amesisitiza kuwa umeme wa Bwawa la Nyerere ni kichocheo cha ukuaji wa uchumi, ajira na maendeleo ya kijamii, akihimiza wananchi kuchangamkia fursa zinazojitokeza ili kuifanya Ruvuma kuwa kitovu cha biashara na uwekezaji wa ukanda wa kusini mwa Tanzania.

Mkoa wa Ruvuma kupitia mto Luegu kutoka wilayani Namtumbo unachangia asilimia 19 ya maji katika mto Rufiji unaotumika katika bwawa la kuzalisha umeme la Mwalimu Nyerere





Muonekano wa mto Ruvuma katika eneo la Angeta ,Namtumbo

SERIKALI KUENDELEA KUWEKA MAZINGIRA WEZESHI KWA NGOs

Serikali imeendelea kusisitiza umuhimu wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) kushirikiana na serikali katika utekelezaji wa ajenda za maendeleo ya taifa kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025–2050.

Akizungumza katika Jukwaa la mwaka la NGOs Mkoa wa Ruvuma, Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa Brigedia Jenerali Ahmed Abbas Ahmed, amesema dira hiyo inalenga kujenga uchumi shindani unaotegemea maarifa, ubunifu, teknolojia na uzalishaji wenye tija.

Amesisitiza kuwa mashirika yanapaswa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na kuandaa mipango kazi inayooana na maono ya taifa.

Naye Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma, Wakili Mary Gasper Makondo, amesisitiza kuwa mashirika yasiyo ya kiserikali yanapaswa kufanya kazi kwa uwazi na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kila baada ya miezi mitatu.

Amesema uwazi huo unapaswa kuendana na uratibu wa karibu na serikali kupitia maafisa maendeleo wa mkoa, halmashauri na wasajili wasaidizi, ili kuhakikisha miradi inawafikia walengwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya kwa jamii.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Mashirika yasiyo ya kiserikali Mkoa wa Ruvuma, Antony Mbilinyi, amesema changamoto kubwa inayoyakabili mashirika ni ushirikiano na taasisi za kifedha, ambapo benki zimekuwa zikichelewesha utekelezaji wa miradi ya kijamii. Amefafanua kuwa kuanzishwa kwa mifuko ya pamoja kupitia mfumo wa CSR na NaCoNGO kunalenga kurahisisha upatikanaji wa fedha za ndani.





HAZINA ILIYOLALA RUVUMA: MITI ILIYOGEUKA MAWE YAWEZA KUFUNGUA UKURASA MPYA WA UTALII RUVUMA

Wakati dunia ikitafuta vivutio vipya vya utalii, Ruvuma ina hazina ambayo haipigi kelele lakini inaweza kuwa na thamani kubwa kisayansi na kiuchumi: mabaki ya miti yaliyogeuka mawe baada ya mchakato wa kijiolojia wa mamilioni ya miaka.

Ndani ya ushoroba wa Selous–Niassa na Pori la Akiba Liparamba, mabaki hayo yameonekana maeneo ya Mpurakacheche na Mbarang'andu, Namtumbo, pamoja na Mbati, Tunduru.

Ngwatura Ndunguru, Mkurugenzi Mstaafu wa Uhifadhi na mwanzilishi wa Pori la Akiba Liparamba, anasema mabaki hayo yanaonesha maumbo ya mashina na matawi ya miti, huku wataalamu wakieleza kuwa madini, ikiwemo silika, yalipenya kwenye tishu za miti na kuzibadilisha kuwa mawe.

Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa na wataalamu wa uhifadhi, ushoroba huo una zaidi ya aina 2,100 za mimea, zikiwemo takribani aina 600 za miti.

Mhifadhi Deborah Emily anaitaja Ruvuma kama eneo lenye upekee mkubwa wa geotourism Kusini mwa Sahara, huku Mhifadhi Maajabu Mbogo akieleza kuwa Liparamba lina mazingira bora ya kuhifadhi urithi huo wa kijiolojia.

Sasa changamoto si uwepo wa hazina hiyo adimu ya utalii badala yake ni kuitambua, kuilinda, kuifanyia utafiti na kuitangaza kimataifa.



CHEMCHEMI NDOGO YA MATOGORO INAYOANZA SAFARI YA MTO RUVUMA HAZINA YA MAJI INAYOUNGANISHA TANZANIA NA MSUMBIJI

Kila alfajiri, chemchemi ndogo inayochomoza kwenye Milima ya Matogoro manispaa ya Songea mkoani Ruvuma huanza safari ambayo watu wengi hawaioni kwa ukubwa wake.

Kutoka hapo ndipo simulizi ya Mto Ruvuma inapoanzia mto unaosafiri zaidi ya kilomita 800 hadi Bahari ya Hindi, ukibeba historia, uchumi, utalii na maisha ya jamii za Tanzania na Msumbiji.

Mratibu wa Utalii Kanda ya Kusini, Deborah Mwakanosya, anasema chanzo cha mto huo kipo katika eneo la Milima ya Matogoro chini ya usimamizi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), na mto huo ni miongoni mwa vivutio muhimu vya utalii Ruvuma.

Thamani yake haipo kwenye maji pekee. Mwambesi, Liparamba, Tulila na Nakatuta zimeibuka kama maeneo yenye fursa za utalii wa mazingira, maporomoko na mandhari za asili.

Takwimu zilizotolewa katika taarifa hii zinaonesha zaidi ya watalii 1,200 walitembelea Mwambesi na Liparamba mwaka 2024.

Historia kubwa zaidi: maeneo ya Mto Ruvuma yalihusishwa na harakati za kupinga ukoloni na baadaye yakawa sehemu muhimu katika historia ya ukombozi wa Msumbiji.

Daraja la Umoja, Mtambaswala, limeongeza maana nyingine Mto Ruvuma si mpaka tu; ni daraja la biashara, watu na diplomasia kati ya Tanzania na Msumbiji.

Chemchemi ndogo ya Matogoro, ni mwanzo wa simulizi ambayo bado haijaandikwa kikamilifu katika ramani ya utalii wa Afrika Mashariki.





DC MASANJA ATOA DEADLINE YA SIKU 34: MIRADI YA ELIMU NA AFYA LIGUNGA IKAMILIKE



Saa ya utekelezaji imeanza Ligunga. Mkuu wa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma Mheshimiwa Denis Masanja, ameagiza hadi Oktoba 6, 2026 kukamilika kwa miradi ya maendeleo aliyokagua katika Kata ya Ligunga wilaya ya Tunduru

Katika ziara hiyo, DC Masanja alikagua Shule ya Awali Samaria katika Kijiji cha Mtengashari, Shule ya Sekondari Ligunga na Zahanati ya Mtengashari, akisisitiza kasi, ubora wa kazi na matumizi sahihi ya rasilimali.

Kutoka Septemba 2 hadi Oktoba 6 ni takribani siku 34 muda ambao sasa umewekwa kama kipimo cha uwajibikaji kwa wasimamizi wa miradi hiyo.

“Nataka ifikapo tarehe 6 Oktoba 2026 miradi hii iwe imekamilika na iwe tayari kuanza kutumika kwa wananchi,” amesema DC Masanja.

kukamilika kwa miradi hiyo kunalenga kuboresha mazingira ya elimu kwa watoto na wanafunzi, huku Zahanati ya Mtengashari ikitarajiwa kuongeza upatikanaji wa huduma za afya kwa wananchi wa Mtengashari na maeneo jirani.



Muonekano wa Maporomoko ya Nakatuta katika mto Ruvuma ndani ya pori la Liparamba

SH. BILIONI 1.5 ZAGEUKA HUDUMA ZA MAJI, AFYA RUVUMA

Zaidi ya Sh. bilioni 1.5 zimeelekezwa katika miradi ya maji, usafi wa mazingira na afya wilayani Tunduru na Namtumbo mkoani Ruvuma, huku utekelezaji wake ukifuatiliwa kwa karibu kuhakikisha fedha hizo zinageuka kuwa huduma halisi kwa wananchi.

Timu ya Utekelezaji na Ufuatiliaji ya Huduma Endelevu za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (SRWSSP), Awamu ya Pili, kwa ufadhili wa Benki ya Dunia, imekagua miradi mbalimbali, ikiwemo Mradi wa Maji Hulia, Tunduru, wenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 1.36.

Meneja wa RUWASA wilaya ya Tunduru Mhandisi Maua Mgalla amesema mradi huo umekamilika Mei 2025 na vituo vyake sita vya Prepaid vyote vinafanya kazi.

Namtumbo, wananchi 860 wa Kijiji cha Kilimasera wameanza kunufaika na Mradi wa Maji Kilimasera uliogharimu Sh. milioni 60, baada ya kukamilika Machi 2025.

Meneja wa RUWASA Namtumbo, Mhandisi David Mkondya, amesema mradi huo ulianza Septemba 2024 na ulihusisha uchimbaji wa kisima chenye kina cha mita 143, ufungaji wa mota na pampu, tenki la kuhifadhi lita 10,000, pamoja na vituo vitano vya kuchotea maji na kituo katika Shule ya Msingi Kilimasera.

Amesema huduma hiyo imepunguza muda ambao wananchi walitumia kwenda mito kutafuta maji, hivyo kuwawezesha kutumia muda huo katika shughuli za uzalishaji na kuwawezesha watoto kufika shuleni kwa wakati.





USHURU WA MAKAA YA MAWE WAGEUKA AJENDA KUU MBINGA

Wakati makaa ya mawe yakiendelea kuwa sehemu muhimu ya shughuli za kiuchumi wilayani Mbinga, Mkoani Ruvuma Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imewataka wasafirishaji na kampuni zinazojihusisha na biashara hiyo kutekeleza wajibu wao wa kisheria kwa kulipa ushuru na madeni ya Serikali kwa wakati.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Joseph Kashushura, ametoa msisitizo huo katika kikao kazi na wawakilishi wa makampuni na wadau wa maendeleo wanaojihusisha na usafirishaji wa makaa ya mawe.

Kashushura amesema ukusanyaji wa mapato ya ndani ni nguzo ya utekelezaji wa huduma na miradi ya maendeleo, ikiwemo afya, elimu, maji na barabara.

“Nimewaita hapa kuwakumbusha madeni ya ushuru mnayodaiwa; muanze kuyalipa mara moja kulingana na taratibu zilizowekwa ili nasi tutekeleze miradi ya maendeleo,” amesema Kashushura.

Ameonya kuwa Serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki ya uwekezaji, lakini itachukua hatua za kisheria dhidi ya kampuni zitakazokiuka taratibu za ulipaji wa ushuru.

Wadau hao wameahidi kushirikiana na Halmashauri kuhakikisha madeni yanalipwa na matakwa ya sheria yanazingatiwa





MBAAZI ZOTE ZAMALIZIKA MNADANI MTINA: MKULIMA APATA SH1,260 KWA KILO

Mbaazi za wakulima wa Mtina wilayani Tunduru mkoani Ruvuma zimepata soko lote katika mnada wa pili, huku bei ikifika hadi Sh1,260 kwa kilo na wastani wa Sh1,237.

Takwimu za mnada huo zinaonesha bei ya chini ilikuwa Sh1,200 kwa kilo, ikimaanisha tofauti ya Sh60 kati ya bei ya juu na ya chini. Muhimu zaidi, mbaazi zote zilizoletwa mnadani ziliuzwa.

Mnada umeendeshwa kupitia mfumo wa mauzo ya kidijitali chini ya usimamizi wa Soko la Bidhaa Tanzania, mfumo unaowawezesha wanunuzi kushindana kwa bei badala ya mkulima kutegemea mnunuzi mmoja.

Kwa mtazamo wa masoko ya kilimo, ushindani huo unaweza kuongeza uwazi wa bei na kuboresha uwezo wa mkulima kujua thamani ya bidhaa yake kabla ya kuuza.



UNITI 42 ZA DAMU ZAFIKISHWA HOSPITALI YA RUFAA SONGEA

Wakati mahitaji ya damu hospitalini yakiendelea kuhitaji ushiriki wa jamii, Taasisi ya Waislamu JAI imeonesha kwa vitendo kuwa dakika chache za mtu mmoja zinaweza kuwa mwanzo wa kuokoa maisha ya mwingine.

JAI imechangia uniti 42 za damu katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea, baada ya kushiriki zoezi la uhamasishaji wa uchangiaji damu lililofanyika kwa siku mbili, Agosti 28 hadi 29, 2026, katika Viwanja vya Soko Kuu Songea.

Zoezi hilo lililobeba ujumbe “CHANGIA DAMU, OKOA MAISHA” liliwalenga wafanyabiashara, wananchi na watumiaji wa soko, likisisitiza umuhimu wa kuwa na akiba ya damu ya kutosha kwa wagonjwa wanaohitaji huduma za dharura na matibabu mbalimbali.

Waandaaji wamesema ushiriki wa taasisi kama JAI ni sehemu muhimu ya kuimarisha upatikanaji wa damu na kuongeza mwitikio wa jamii katika shughuli za kuokoa maisha.





Muonekano wa mti mawe Kijiji cha Mbati ,wilaya ya Tunduru

WANAFUNZI WA SKILL PATH WAGEUZA WODI YA HOSPITALI YA SONGEA KUWA SEHEMU YA FURAHA

Si kila dawa huja kwenye chupa wakati mwingine, huja kupitia moyo wa mtoto.

Wanafunzi wa Skill Path English Medium Primary School ya manispaa ya Songea mkoani Ruvuma wamefanya ziara ya kijamii katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea, wakitoa zawadi na faraja kwa wagonjwa waliolazwa hospitalini hapo.

Afisa Muuguzi Msaidizi aliyekuwa Msimamizi wa zamu, Sairice Mbena, alisema ziara hiyo imewapa wagonjwa faraja, matumaini na moyo wa kuendelea kupambana na changamoto za kiafya.

"Tunashukuru sana uongozi wa Skill Path kwa kufikiri kuwatembelea wagonjwa wetu," alisema Mbena.

Kwa upande wake, Mwalimu Mkuu wa Skill Path English Medium Primary School, Rashidi Ayasi, alisema lengo la ziara hiyo ni kuwafundisha watoto upendo kwa vitendo, kuwajali wengine na kushiriki katika shughuli za kijamii.

Ziara hiyo inaonesha kuwa elimu bora si darasani pekee; inajenga pia kizazi kinachojua kuhurumia, kusaidia na kugusa maisha ya wengine.







MIRADI YA BILIONI 2.06 YAKAGULIA SONGEA MANISPAA

Timu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkoa wa Ruvuma imekagua miradi sita yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 2.06 katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea, ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na ukamilishaji.

Timu hiyo ikiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Sunday Hebuka, imekagua mradi wa ujenzi wa Shule ya Awali na Msingi ya Amali wenye thamani ya shilingi milioni 344.9, pamoja na ujenzi wa vizimba na choo katika stendi ya Ruhuwiko wenye thamani ya shilingi milioni 101.9.

Miradi mingine ni ukamilishaji wa Zahanati ya Matarawe yenye thamani ya shilingi milioni 120, ujenzi wa jengo la Benki ya NMB Msamala wenye thamani ya shilingi milioni 426.4, pamoja na ujenzi wa jengo jipya la Halmashauri ya Manispaa ya Songea lenye thamani ya shilingi bilioni 1.

Vilevile, ukaguzi huo umehusisha pia ujenzi wa bweni la Shule ya Sekondari Chandarua lenye thamani ya shilingi milioni 70, mradi ambao unatarajiwa kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa bweni.

Akizungumza kwa niaba ya timu ya wataalam, Hebuka ameelekeza kuwa miradi hiyo ikamilishwe kwa kasi na kwa kuzingatia ubora unaohitajika, akibainisha kuwa utekelezaji wa viwango sahihi vya ujenzi ni muhimu ili kulinda thamani ya fedha za Serikali na kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kwa wakati





SIRI YA VIHENGE VYA CHAKULA VILIVYOMFICHA NYERERE NAMTUMBO HAPA NDIPO WANANCHI WA KAWAIDA WALILINDA NDOTO YA UHURU

Mwaka 1955, wakati wakoloni wakimtafuta Mwl. Julius Kambarage Nyerere usiku na mchana, kijiji cha Luegu wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma, kiligeuka kuwa ngome ya siri ya harakati za uhuru.

Kwa siku mbili, Nyerere alifichwa kwenye vihenge vya chakula vya familia ya Maulid Hassan Mang'unyuka kama anavyoonekana kwenye picha aliyekuwa kijana wa miaka 20. "Askari walikuwa wakizunguka kila kona. Nilimpeleka kwenye vihenge vya baba yangu," anakumbuka Mzee Mang'unyuka, ambaye leo ana miaka zaidi ya 90.

Ndani ya maficho hayo, chakula kilishirikishwa, mipango ya harakati ikaendelea na hofu ikageuka kuwa ujasiri.

Tukio hilo linaonesha upande ambao mara nyingi hauonekani katika historia: uhuru wa Tanganyika haukujengwa mijini pekee; ulilindwa pia na wananchi wa vijijini.

Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo, Ngollo Malenya, anasema eneo hilo ni sehemu ya urithi unaoweza kuunganisha historia na utalii.

Miaka 70 baadaye, vihenge hivyo vinabaki na ujumbe mmoja: wakati mwingine historia ya taifa huokolewa na watu ambao majina yao hayakuandikwa vitabuni.







WAGANGA WA TIBA ASILI WATAKIWA KUJISAJILI, NI 10 PEKEE WENYE LESENI

Takribani wataalamu 375 wa tiba asili na tiba mbadala wanapatikana Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma lakini ni 10 pekee wenye usajili na leseni, huku wengine 40 wakiwa na usajili wa muda hali iliyosababisha Serikali kutoa wito wa kuongeza kasi ya usajili.

Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Peres Magiri, amewataka wataalamu hao kujisajili kupitia Mfumo wa Usajili na Utoaji Leseni kwa Watoa Huduma za Afya (HPRS) ili watambulike rasmi na kurahisisha usimamizi wa shughuli zao.

Akizungumza katika kilele cha Wiki ya Tiba Asili na Tiba Mbadala wilayani humo, Magiri amesema Serikali inatambua mchango wa tiba asili katika sekta ya afya na inawataka wataalamu kutumia teknolojia ya kisasa huku wakizingatia sheria, kanuni na miongozo.

Pia amewataka kuacha kuwalaghai wateja na kujihusisha na vitendo vya kishirikina, ikiwemo ramli chonganishi, pamoja na kuwa waangalifu dhidi ya wateja wenye viashiria vya uhalifu au uvunjifu wa amani.

Kaimu Katibu wa Chama cha Wataalamu wa Tiba Asili Nyasa, Salmon Komba, ameahidi ushirikiano na Serikali.





Muonekano wa mnara wa makumbusho ya Taifa majimaji wa mashujaa 67



MBINGA DC YAWEKA MKAZO USALAMA WA NYAMA

Usalama wa nyama hauanzi kwenye sahani ya mlaji; unaanzia machinjioni. Hilo ndilo lililosisitizwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha wachinjaji, wamiliki wa mabucha na wauza nyama.

Mkuu wa Divisheni ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mhandisi Evance Haule, aliwataka wadau kushirikiana kwa karibu na wataalamu wa mifugo, huku akisisitiza nyama inayouzwa iwe imekaguliwa na kuthibitishwa kuwa salama kwa matumizi ya binadamu.

Haule pia alitaka kuimarishwa kwa usafi wa machinjio, vyombo vya usafirishaji na mabucha, pamoja na kuhakikisha vibali vinavyotakiwa vinapatikana na ushuru wa Halmashauri unalipwa kwa wakati.

Afisa Mifugo Haruna Masige alisema umoja wa wadau ni muhimu katika kutatua changamoto zao kwa kushirikiana na Halmashauri.

Katika uchaguzi wa viongozi, Hance Turuka alichaguliwa Mwenyekiti, Zandati Mdegela Mwenyekiti Msaidizi, huku Patrick Patrick akiwa Katibu, Baltazary B. Nchimbi Katibu Msaidizi na Baraka Mbena Mtunza Hazina



TIMU YA UFUATILIAJI RUVUMA YAKAGUA MIRADI YA ZAIDI YA BILIONI 1.5

Timu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkoa wa Ruvuma imekagua miradi saba ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 1.5 katika Halmashauri ya Wilaya ya Songea, ambayo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Timu hiyo ikiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Sunday Hebuka, imekagua mradi wa ujenzi wa kituo cha afya Peramiho wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 641.6, pamoja na ujenzi wa matundu 21 ya vyoo katika Shule ya Msingi Mnyonga yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 49.4.

Vilevile, imekagua ujenzi wa madarasa mawili, matundu 12 ya vyoo na ukarabati wa Shule ya Msingi Mnyonga wenye thamani ya shilingi milioni 131.8, pamoja na ujenzi wa matundu mawili ya vyoo katika Shule ya Sekondari Namihoro wenye thamani ya shilingi milioni 3.4.

Ukaguzi huo umehusisha pia ujenzi wa madarasa sita, matundu 10 ya vyoo na mabweni mawili katika Shule ya Sekondari Jenista Mhagama wenye thamani ya shilingi milioni 417, ujenzi wa kituo cha afya Mpandangindo wenye thamani ya shilingi milioni 250, pamoja na ujenzi wa matundu sita ya vyoo katika Shule ya Msingi Kituro wenye thamani ya shilingi milioni 10.2.

Akizungumza kwa niaba ya timu ya wataalam, Hebuka ameagiza kasi na ubora katika utekelezaji wa miradi hiyo, akisisitiza kuwa viwango vya ujenzi vinapaswa kuzingatiwa ili kuhakikisha thamani ya fedha za Serikali inalindwa na wananchi wanapata huduma bora kwa wakati.







VIJANA RUVUMA WAFUNDISHWA KUBADILI TAKA KUWA CHAKULA CHA MIFUGO NA MBOLEA

Taka za kikaboni ambazo mara nyingi huonekana kuwa mzigo kwa mazingira sasa zinaweza kuwa chanzo cha ajira, kipato na biashara mpya kwa vijana wa Ruvuma kupitia teknolojia ya Inzi Chuma, maarufu kama Black Soldier Fly (BSF).

Vijana mkoani humo wamepatiwa mafunzo na taasisi isiyo ya kiserikali ASERACA, yaliyofanyika Songea Club, kuhusu namna ya kutumia BSF kuchakata taka za kikaboni na kuzibadilisha kuwa chakula cha mifugo na mbolea.

Mafunzo hayo yamewajengea vijana ujuzi wa kukusanya na kuchambua taka, kuzalisha na kutunza Inzi Chuma, pamoja na kutumia mabaki yake kuzalisha bidhaa zenye thamani kwa kilimo na ufugaji.

Kinachovutia zaidi ni kwamba fursa haishii kwenye ufugaji wa Inzi Chuma. Mnyororo mzima wa thamani unafungua nafasi za kukusanya taka, kuchambua, kutengeneza trei na vifaa vya ufugaji, kuanzisha mashamba ya maonesho, kuzalisha chakula cha mifugo, kutengeneza mbolea, masoko na usambazaji.

Kwa mtazamo wa uchumi wa mzunguko, teknolojia hii inabadilisha taka kutoka kuwa gharama ya utupaji na kuwa malighafi yenye thamani ya kiuchumi.



POLISI NA WANANCHI RUVUMA WAUNGANA KUPAMBANA NA UHALIFU



Michezo imegeuka kuwa daraja jipya kati ya Polisi na wananchi wa Ruvuma, huku Jeshi la Polisi likitumia Bonanza la Polisi Jamii Cup kuimarisha amani, upendo na ushirikiano katika jamii.

Akizungumza katika Uwanja wa Majimaji, Songea, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, SACP Marco Chilya, alisema michezo si burudani pekee, bali ni nyenzo ya kujenga mahusiano na kuongeza ushirikiano katika kuzuia na kudhibiti uhalifu.

Bonanza hilo liliandaliwa kuelekea miaka 20 ya Polisi Jamii, likihusisha mpira wa miguu, riadha za mita 100 na 200 kwa wanawake na wanaume pamoja na kuvuta kamba, huku wananchi na askari wakishiriki pamoja.

Katika soka, sekondari ya Emmanuel Nchimbi iliifunga Songea Boys 1-0, kabla ya FFU Ruvuma kutwaa kombe baada ya kuishinda Polisi Wilaya ya Nyasa .

Washiriki walikabidhiwa medali, mipira na kombe.

Kwa mujibu wa SACP Chilya, ushirikiano wa Polisi na wananchi ni msingi wa jamii salama ambapo amesisitiza Michezo inaweza kuwa chachu ya kuimarisha mshikamano na kuongeza ufanisi katika mapambano dhidi ya uhalifu.



PERAMIHO: HAZINA YA MIAKA 128 INAYOHIFADHI HISTORIA YA TANZANIA NA ULAYA



Kilomita 24 kutoka Songea mjini mkoani Ruvuma, kuna mji mashuhuri wa Peramiho eneo ambalo zaidi ya miaka 128 limebeba historia ya dini, elimu, afya, utamaduni na uhusiano wa Tanzania na Ulaya.

Safari ya Peramiho ilianza 31 Julai 1898, wakati Padre Cassian Spiß, OSB, kutoka Wabenediktini wa St. Ottilien, Ujerumani, alipoanzisha kituo cha misheni Peramiho. Kwa mujibu wa historia ya Wabenediktini, misheni hiyo ilipanuka na kuwa kituo cha elimu, afya na huduma za kijamii. Watawa wa kike walifika Peramiho mwaka 1901, wakianzisha shule na huduma za afya.

Peramiho pia ilipitia machungu ya Vita ya Maji Maji (1905–1907), ambapo kituo cha misheni kiliharibiwa. Baadaye kilijengwa upya na kuendelea kukua.

Alama kubwa zaidi ni Kanisa la tatu kujengwa la Abasia ya Peramiho ambalo ujenzi wake ulifanyika 1943–1948 chini ya Abate Askofu Gallus Steiger, OSB.

Leo, Peramiho si historia iliyoganda; ni rasilimali hai ya utalii wa kitamaduni inayoweza kuunganisha historia, usanifu, dini na urithi wa Tanzania. Peramiho ni mahali ambapo historia haisimuliwi tu badala yake inaonekana, inaguswa na bado inaendelea kuishi.



WATALII WA MAREKANI WALIVYOVUTIWA NA UTALII WA MTO RUHUHU NA ZIWA NYASA



Ruvuma sasa inalenga kugeuza uzuri wa Mto Ruhuhu na Ziwa Nyasa kuwa kivutio cha kimataifa baada ya waongoza watalii sita kutoka Marekani kutembelea maeneo hayo na kuridhia kuanza kuleta watalii kutoka nchi mbalimbali.

Wageni hao, wanaomiliki kampuni za kimataifa za utalii za Dorobo Tours, ABD Safari na Offmap Tours, wamevutiwa zaidi na fursa za kuteleza na mitumbwi Mto Ruhuhu, pamoja na utalii wa kupiga picha za samaki wa mapambo ndani ya Ziwa Nyasa.

Utafiti unaonesha kuwa , Mto Ruhuhu huchangia takribani asilimia 20 ya maji yanayoingia Ziwa Nyasa, huku Ziwa Nyasa likitajwa kuwa na takribani aina 400 za samaki wa mapambo rasilimali inayoweza kuongeza bidhaa mpya katika utalii wa Tanzania.

Kabla ya ziara hiyo, wageni hao waliripoti katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma kwa ajili ya kujitambulisha, kisha wakaendelea kutathmini fursa za utalii katika mkoa wa Ruvuma.





JESHI LA MAGEREZA TUNDURU LAGEUKA KUWA NGUVU YA UHAI: USAFI HOSPITALINI NA DAMU KWA WAGONJWA

Katika kuadhimisha miaka 65 ya Jeshi la Magereza tangu Uhuru wa Tanzania, Gereza la Wilaya ya Tunduru na Gereza la Majimaji mkoani Ruvuma wameunganisha uzalendo na huduma kwa jamii kwa kufanya usafi katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru na kuchangia damu.

Mkuu wa Gereza Tunduru, SSP. Uswege Yoram, amesema hatua hiyo inaakisi dhamira ya Jeshi la Magereza ya kushirikiana na jamii na kushiriki shughuli zenye manufaa kwa Taifa.

Watumishi hao wamesafisha maeneo mbalimbali ya hospitali, huku wakitoa damu kwa ajili ya kusaidia wagonjwa wanaohitaji huduma za dharura na tiba zinazotegemea upatikanaji wa damu salama.

Uongozi wa Hospitali ya Wilaya ya Tunduru umelishukuru Jeshi la Magereza na kuhamasisha wananchi kujitokeza kuchangia damu kwa hiari



WAFUGAJI NA WATAALAM RUVUMA WAANZA MAFUNZO UFUGAJI INZI CHUMA

Wafugaji na wataalam mkoani Ruvuma wameanza mafunzo ya ufugaji wa wadudu aina ya inzi chuma (Black Soldier Flies) kama mbadala wa chakula cha mifugo.

Wadudu hao wanatajwa kuwa na protini nyingi na kuzalishwa kwa gharama nafuu kupitia taka za sokoni na majumbani.

Mafunzo hayo ya siku 4 yameratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu na kutolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya ASARECA, na kufanyika katika ukumbi wa Songea Club.

Lengo ni kuwawezesha vijana kupata ujuzi wa kuzalisha inzi chuma ili kupunguza gharama za chakula cha mifugo na kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja na vikundi.

Akifungua mafunzo hayo, Katibu Tawala Msaidizi – Uchumi na Uzalishaji, Deodatus Sibula, amewataka wananchi na vijana kutumia teknolojia hiyo kama fursa ya ajira na kipato.

Amesema karibu asilimia 60 ya gharama za ufugaji hutumika kwenye chakula, hivyo njia hii itakuwa chachu ya kuboresha sekta ya ufugaji mkoani Ruvuma.

Kwa upande wake, Afisa Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Godfrey Christopher, amesema mafunzo hayo ni sehemu ya programu ya IFAD inayotekelezwa katika mikoa 11 na halmashauri 41 nchini. Amesisitiza kuwa teknolojia hiyo inasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia taka badala ya kutegemea mvua kama ilivyo kwa kilimo cha soya.

Naye Afisa Uvuvi Mfawidhi wa Kituo cha Ruhila, Luka Mgwena, amesema kituo hicho kimepata nafasi ya kufundisha vijana namna ya kuchakata taka za sokoni na kuzibadilisha kuwa chakula cha mifugo na mbolea ya asili.



WANANCHI WAONYWA KUTUPA TAKA KWENYE MITARO SONGEA



Hofu ya mvua nyingi msimu huu imeibua tahadhari mpya kwa wananchi wa Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma baada ya mamlaka kuwaonya kuhusu tabia ya kutupa taka kwenye mitaro ya kupitisha maji.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Mhe. Kapenjama Ndile, amesema taka zinazoziba mitaro zinaweza kusababisha maji kujaa na kuingia kwenye makazi, hali inayoweza kuongeza hatari ya magonjwa ya mlipuko.

Akizungumza wakati wa zoezi la usafi katika Soko la Samaki na Dagaa la Mfaranyaki, Ndile amewataka wafanyabiashara na wananchi kuacha kutumia mitaro kama sehemu ya kutupa taka.

“Usafi wa mitaro ni kinga ya moja kwa moja dhidi ya mafuriko na hatari za kiafya,” ujumbe wa mamlaka ukisisitiza umuhimu wa uwajibikaji wa wananchi.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea, Wakili Bashir Mhoja, amesema hali ya usafi, hasa kwenye mitaro ya maji, bado hairidhishi.

Manispaa imeanza maandalizi ya kampeni ya siku 94 za usafi ili kuboresha mazingira na kuimarisha afya ya wananchi.





HOSPITALI MBILI, UZOEFU MMOJA: SONGEA NA SOKOINE WASHIRIKI MBINU ZA KUBORESHA HUDUMA

Ziara ya kikazi ya uongozi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi – Sokoine katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Songea imeibua mkakati mpya wa kubadilishana uzoefu na mbinu za kuboresha huduma kwa wananchi.

Akiongoza ujumbe huo, Mganga Mfawidhi wa Sokoine RRH, Dkt. Alexander Makalla, alitembelea idara ya Magonjwa ya Dharura (Emergency Department) na huduma ya kusafisha damu (Dialysis), akishuhudia namna watumishi wanavyotumia miundombinu ya kisasa kuwahudumia wagonjwa.

“Tumejifunza kitu kikubwa kupitia miundombinu mlizonazo na tutaenda kuimarisha na kuboresha huduma zetu kwa wananchi,” alisema Dkt. Makalla.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Songea RRH, Dkt. Hassan Lumbe, amesema hospitali hiyo iko tayari kushirikiana katika kubadilishana maarifa na uzoefu.

Ziara hii inalenga maeneo mawili muhimu huduma za dharura na dialysis ambayo yanahitaji miundombinu, teknolojia na wataalamu wenye uwezo.

Kwa hospitali za umma, kubadilishana maarifa ni uwekezaji unaoweza kubadilisha matokeo ya huduma za afya.



VIONGOZI WA DINI WAKUTANA TUNDURU KUJENGA DARAJA LA AMANI NA MSHIKAMANO



Viongozi wa dini mbalimbali wilayani Tunduru Mkoani Ruvuma wameungana kupitia Mradi wa Mshikamano, katika hatua inayolenga kuimarisha amani, upendo, kuheshimiana na ushirikiano miongoni mwa waumini wa madhehebu tofauti.

Ziara hiyo iliyoongozwa na Ebenenze imewakutanisha viongozi wa dini kwa majadiliano kuhusu namna ya kutumia nafasi yao kuimarisha umoja na kudumisha utulivu katika jamii.

Katika hatua nyingine, viongozi hao walitembelea nyumba mbalimbali za ibada zilizopo Tunduru, wakilenga kujenga uelewano wa karibu kati ya viongozi na waumini wa madhehebu mbalimbali.

Mradi huo unaendesha ujumbe wake kupitia kauli mbiu “Dini mbalimbali, Upendo, Amani na Mshikamano,” ukiweka mkazo kwenye ushirikiano badala ya tofauti za kidini.

Tunduru inaonesha kuwa tofauti za imani si lazima ziwe mipaka; zinaweza kuwa daraja la kujenga jamii yenye amani, heshima na mshikamano.

USAFI JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI TUNDURU

Zoezi la usafi wa Jumamosi ya mwisho wa mwezi limefanyika katika Stendi Kuu na Soko Kuu la Tunduru mkoani Ruvuma likiongozwa na Katibu Tawala wa Wilaya, Milongo Sanga, kwa kushirikiana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Chiza Marando.

Watumishi, wananchi na wadau mbalimbali wameungana katika ukusanyaji wa taka na usafishaji wa maeneo hayo, ikiwa ni sehemu ya kutekeleza maagizo ya Serikali na kuimarisha utamaduni wa usafi wa mazingira.

Akizungumza baada ya zoezi hilo kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala Milongo Sanga amewapongeza washiriki na kusisitiza kuwa usafi haupaswi kusubiri siku ya mwisho wa mwezi.

Ametoa wito kwa wananchi kuepuka utupaji wa taka ovyo na kufanya usafi kuwa sehemu ya maisha ya kila siku, akisisitiza kuwa mazingira safi yanahitaji ushirikiano wa mamlaka, wananchi na wadau wote.



MADIWANI WATAKIWA KUSAIDIA KUPANDISHA UFAULU WA WANAFUNZI MBINGA



Wakati Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma ikifanya vizuri katika maeneo mbalimbali ya maendeleo, elimu imetajwa kuwa eneo linalohitaji nguvu mpya na madiwani wamepewa jukumu la kuwa sehemu ya suluhisho.

Katibu Tawala Wilaya ya Mbinga Pendo Ndumbaro, amesema madiwani wanapaswa kushiriki kikamilifu kufuatilia mazingira ya kujifunzia na maendeleo ya taaluma katika shule za Msingi na Sekondari.

Ndumbaro alitoa kauli hiyo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne ya mwaka 2025/2026.

"Mbinga DC tuko vizuri kwenye maeneo mengine; kwenye elimu tu ndipo panahitaji juhudi za pamoja kuongeza ufaulu," alisema.

Halmashauri tayari imeanza kufanya ziara za shule kukagua mazingira ya ujifunzaji na kufuatilia maendeleo ya kitaaluma.

Ndumbaro amesema ushiriki wa madiwani katika ngazi za kata unaweza kuongeza ufuatiliaji na uwajibikaji, hivyo kuchochea matokeo bora katika mitihani ya kitaifa.

Kwa upande wa mapato, Halmashauri imevuka lengo na kufikia asilimia 120 ya makusanyo, huku makisio ya mwaka 2026/2027 yakiongezwa hadi Sh bilioni 14.



VIJANA 41 RUVUMA WAPATIWA MAFUNZO YA VITENDO KATIKA KITUO CHA UKUZAJI VIUMBE MAJI RUHILA

Vijana 41 kutoka mkoani Ruvuma wamepatiwa mafunzo ya vitendo kuhusu teknolojia ya ufugaji wa inzi chuma (Black Soldier Fly – BSF), ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuwajengea uwezo wa kutumia taka za kikaboni kuzalisha bidhaa zenye thamani na kujipatia fursa za ajira na kipato.

Mafunzo hayo yaliyotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ASERACA, yalihusisha ziara ya mafunzo katika Kituo cha Kuendeleza Ukuzaji Viumbe Maji Ruhila, kilichopo Kata ya Mkuzo, Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma.

Akieleza namna teknolojia hiyo inavyofanya kazi, Afisa Ukuzaji Viumbe Maji wa Kituo cha Ruhila, Victoria Mzamilu, alisema kuna hatua mbalimbali zinazopaswa kufuatwa katika uchakataji wa inzi chuma, ikiwemo ukusanyaji na uchambuzi wa taka za kikaboni ambazo hutumika kama chakula cha inzi hao.

Alisema bidhaa zinazopatikana kupitia teknolojia hiyo zinaweza kutumika kama chakula cha mifugo, wakiwemo samaki, kuku na nguruwe, huku mabaki yake yakitumika kutengeneza mbolea kwa ajili ya kilimo.

Victoria aliongeza kuwa mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha vijana kutumia fursa zilizopo katika jamii ili kujiajiri, kuongeza kipato na wakati huo huo kushiriki katika utunzaji wa mazingira kwa kupunguza taka za kikaboni.

Kwa upande wao, baadhi ya wanufaika wa mafunzo hayo walisema wamepata ujuzi katika maeneo mbalimbali, ikiwemo kukusanya na kuchambua taka za kikaboni, kutengeneza trei na vifaa vya kufugia inzi chuma, kuanzisha na kutunza mashamba ya maonesho, kuzalisha chakula cha mifugo, kutengeneza mbolea, pamoja na kutafuta masoko na kusambaza bidhaa zinazotokana na teknolojia hiyo.



MADIWANI WATAKIWA KUSAIDIA KUPANDISHA UFAULU WA WANAFUNZI MBINGA

Wakati Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma ikifanya vizuri katika maeneo mbalimbali ya maendeleo, elimu imetajwa kuwa eneo linalohitaji nguvu mpya na madiwani wamepewa jukumu la kuwa sehemu ya suluhisho.

Katibu Tawala Wilaya ya Mbinga Pendo Ndumbaro, amesema madiwani wanapaswa kushiriki kikamilifu kufuatilia mazingira ya kujifunzia na maendeleo ya taaluma katika shule za Msingi na Sekondari.

Ndumbaro alitoa kauli hiyo katika kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya nne ya mwaka 2025/2026.

"Mbinga DC tuko vizuri kwenye maeneo mengine; kwenye elimu tu ndipo panahitaji juhudi za pamoja kuongeza ufaulu," alisema.

Halmashauri tayari imeanza kufanya ziara za shule kukagua mazingira ya ujifunzaji na kufuatilia maendeleo ya kitaaluma.

Ndumbaro amesema ushiriki wa madiwani katika ngazi za kata unaweza kuongeza ufuatiliaji na uwajibikaji, hivyo kuchochea matokeo bora katika mitihani ya kitaifa.

Kwa upande wa mapato, Halmashauri imevuka lengo na kufikia asilimia 120 ya makusanyo, huku makisio ya mwaka 2026/2027 yakiongezwa hadi Sh bilioni 14.





NYASA YAFIKISHA ASILIMIA 98 YA WANAFUNZI WANAOPATA CHAKULA SHULENI

Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Mkoani Ruvuma imepiga hatua katika utekelezaji wa Mkataba wa Lishe, huku takwimu zikionesha kuwa wanafunzi 53,587, sawa na asilimia 98, wanapata chakula cha mchana katika shule za msingi na sekondari.

Mafanikio hayo yamebainishwa katika kikao cha Kamati ya Lishe ya Wilaya kilichojadili na kutathmini utekelezaji wa afua za lishe kwa robo ya nne, Aprili–Juni 2026. Kikao kiliongozwa na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, Pasifiki Mhapa.

Taarifa imeonesha pia utekelezaji wa afua mbalimbali, zikiwemo utoaji wa vitamini A na dawa za minyoo, matibabu ya utapiamlo mkali, utoaji wa vidonge vya madini chuma kwa wajawazito pamoja na elimu ya lishe kwa jamii na taasisi mbalimbali.

Katika kilimo, Nyasa imeendelea kuwa na uzalishaji mkubwa wa chakula. Mwaka 2025/26, mavuno yalifikia tani 311,790, dhidi ya mahitaji ya tani 83,327.5 kwa kwa mwaka.



MRADI WA UJENZI WA OFISI YA DC NAMTUMBO

Muonekano wa mradi wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma ambapo serikali imetenga shilingi bilioni moja kuanza kutekeleza mradi huo wa jengo la kisasa.

Timu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Mkoa wa Ruvuma ikiongozwa na Mkuu wa Kitengo hicho Sunday Hebuka imekagua mradi huo na kuelekeza kuongeza kasi ya utekelezaji kwa kuzingatia viwango na ubora unaoendana na thamani ya fedha



JENGO HILI LINAFICHA SIRI YA "SIMBA WA VITA" NDANI YAKE KUNA HISTORIA AMBAYO KILA MTANZANIA ANAPASWA KUIONA

Kuna nyumba ambayo ukifungua mlango wake, huingii tu kwenye jengo; unaingia ndani ya historia ya Tanzania.

Hiyo ni Makumbusho ya Dkt. Rashid Mfaume Kawawa yaliyopo Bombambili, mjini Songea mkoani Ruvuma mahali ambapo nguo, samani, picha, medali na vitabu vya kiongozi huyo vimehifadhiwa. Lakini kinachovuta zaidi ni handaki la siri lililohusishwa na maficho ya kipindi cha mapambano ya ukombozi.

Makumbusho hayo yalizinduliwa rasmi 27 Februari 2017, siku ya kumbukumbu ya kuzaliwa Kawawa, baada ya familia yake kukabidhi nyumba hiyo kwa Makumbusho ya Taifa mwaka 2015.

James Mfikwa, Mhifadhi Kiongozi wa Makumbusho ya Dkt. Kawawa, anasema kila chumba kina simulizi inayobeba sehemu ya historia ya taifa.

Zaidi ya watu 8,000 walitembelea makumbusho hayo kati ya 2021 na 2024, kwa mujibu wa takwimu zilizotajwa kutoka Makumbusho ya Taifa.

Kawawa, aliyezaliwa 27 Februari 1926, alikuwa Waziri Mkuu wa Tanganyika na baadaye Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Alifariki 31 Desemba 2009, akiwa na miaka 83.

Urithi wake sasa unaishi Songea si kama kumbukumbu iliyofungwa kwenye vitabu, bali kama historia inayoweza kuonekana, kuguswa na kujifunzwa.



MTO ULIOKUWA CHANZO CHA HOFU SASA WAGEUKA LANGO LA MAENDELEO

Kwa miaka mingi, Mto Ruvuma kwa wakazi wa Mitomoni wilayani Nyasa,ulikuwa kizuizi cha safari, biashara na wakati mwingine maisha. Leo, picha hiyo imebadilika: Daraja la Mitomoni limekamilika kwa asilimia 100, likifungua njia salama ya usafiri na biashara.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mkalawa, Zuberi Mkachaga, anasema wananchi walipoteza ndugu na mali wakati wa kuvuka mto, huku wagonjwa wakilazimika kusubiri au kusafiri zaidi ya kilomita 140 kutafuta huduma za afya.

Daraja hilo lenye urefu wa mita 45, upana wa mita 11.85 na uwezo wa kubeba zaidi ya tani 150, limegharimu Sh bilioni 9.29. Mradi ulianza Novemba 7, 2024 na kutekelezwa na Ovans Construction Limited chini ya usimamizi wa TANROADS.

Meneja wa TANROADS Ruvuma, Mhandisi Salehe Juma, anasema hadi Juni 7, 2026 kazi ilikuwa imekamilika kwa asilimia 100. Mradi pia umejumuisha kilomita 8.8 za barabara za maingilio, mifereji ya maji yenye urefu wa kilomita 2.6 na taa za barabarani.

Mhandisi Juma anasema Mradi ulihusisha wafanyakazi 140, ambapo asilimia 90 walitoka vijiji vya jirani ishara kwamba daraja hilo limejenga ajira na ujuzi.

Kutoka kivuko cha hofu hadi daraja la fursa: Mitomoni sasa inaunganisha watu, masoko na matumaini



JARIDA HILI LIMEANDALIWA NA SEKRETARIETI YA MKOA WA RUVUMA
Kupitia kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma

S.L.P 74 SONGEA
57180 RUVUMA
SIMU Nambari; 025-22602256/2602238
FAX Na.2602144
E-EMAIL: ras.ruvuma@tamisemi.go.tz
TOVUTI: www.ruvuma.go.tz
INSTAGRAM: rs Ruvuma
FACEBOOK: rs Ruvuma
YOUTUBE: rs ruvuma